PORTLAND PARKS & RECREATION

Healthy Parks, Healthy Portland

Sera za Kutunza Shamba la Jamii

1. Umeruhusiwa kulima shamba lako wakati wote wa mwaka. Wakati wa msimu mkuu wa kilimo (Aprili –Oktoba) onyesha kuwa unatumia shamba lako kwa:
   - Kutayarisha udongo ili upande.
   - Kupanda na kukuza mimea.
   - Kuvuna zao lililo tayari.
   - Kuondoa magugu, hasa wakati wa kutoa maua au mimea kuzaa mbegu.
   - Kuvuna nafaka unayotaka kuhifadhi kabla haijamwagika kwenye udongo.

2. Kama haulimi shamba lako kama kawaida, litunze kwa:
   - Kupalilia ili kuondoa magugu, hasa kama magugu yana maua au mbegu.
   - Kung'oa mimea iliyokauka au inayokauka, hasa kama ina magonjwa au imevamiwa na wadudu.
   - Kupanga vitu ambavyo hutumiwa baada ya muda mrefu kama vile visanduku vya nyanya, vijiti, na mbao ambazo hazitumiki.

3. Ni kazi yako kupalilia njia na ukingo wa nyua zilizoko kando ya shamba lako.
   - Hakikisha kwamba njia zilizoko kando ya shamba lako zina upana wa futi 2.5-3 ili wengine waweze kupitia kwa usalama.
   - Palilia njia hizo na nje ya ua kama shamba lako liko karibu na ua.
   - Weka vitu katika shamba lako.
   - Panda mimea ndani ya mipaka ya shamba lako.

4. Portland Parks & Recreation haipeani huduma ya kuzoa taka. Ni kazi yako kushughulikia taka inayotoka kwenye shamba lako.
   - Unaweza kuchanganya mimea kuwa mbolea shambani mwako, uizike au uitupe kwenye pipa la taka la nyumbani.
   - Usitupe taka ovyo nje au ndani ya shamba lako.

5. Usiruhusu wanyama aina ya panya na wadudu wanaouma watu kujenga makao katika shamba lako.
   - Ondoa marundo ya vifusi na ugeuze mbolea yako mara kwa mara.
   - Ondoa chakula kinachovutia wanyama hao kwa kuvuna wakati kiko tayari na kuacha mabaki ya chakula jikoni nyumbani mwako.
   - Mwaga maji yaliyotulia kwa zaidi ya siku 3 ili kuzuia mbu kutaga mayai.

6. Mashamba ya kikaboni yanahitajika.
   - Tumia mbolea na dawa za kikaboni za kuulia wadudu na magugu.
   - Kama huna uhakika kwamba bidhaa unayotaka kutumia imeruhusiwa, itafute kwenye tovuti ya Taasisi ya Mapitio ya Bidhaa za Kikaboni www.omri.org au upige simu kwa Mkulima Mkuu kwa 503-655-8631.

7. Shughulikia shamba lako la jamii kwa angalau masaa 6 kwa mwaka. Ni lazima uwe umehudumu kwa masaa 3 ifikapo tarehe 30 Juni na jumla ya masaa 6 ifikapo 31 Oktoba.
   - Ongea na meneja wa shamba lako akupe orodha ya shughuli zitakazohesabiwa kama kazi ulizojitolea kufanya au soma Maswali yanayoulizwa mara kwa mara.

- Ikiwa huwezi kujitolea kufanya kazi kwa sababu ya ulemavu au shida nyingine ya kibinafsi, ongea na wafanyakazi ili wakuruhusu.
- Wakulima ambao hawatafanya kazi kwa masaa itakikanayo au kuomba ruhusa kwa miaka 2 mfululizo hawataruhusiwa kujisajili tena na watanyang'anywa shamba lao.

Uwajibikaji wa Mkulima na Utekelezaji wa Sera

Ni kazi ya wakulima kuzingatia sera za shamba. Wafanyakazi na meneja wa shamba watasimamia mashamba mwaka wote. Ikiwa mkulima hafuati sera za shamba, wafanyakazi watamkumbusha.

- Ikiwa shamba litakuwa halijashughulikiwa wakati wa msimu wa kilimo (Aprili – Oktoba), wafanyakazi watamtafuta mwenye shamba hilo. Mwenye shamba ana wiki 2 za kujibu na kuanza kulima. Kama shamba halitakuwa limeshughulikiwa baada ya wiki 2, mtu mwingine atapewa shamba hilo.
- Mkulima akipewa kumbusho la tatu wakati wa msimu wa kulima, ana uhuru wa kuingia katika kipindi cha majaribio ambapo watafanya kazi na wafanyakazi na kupanga mpango wa shamba ili kuwawezesha kubaki na shamba lao.
- Wakulima watakaokumbushwa mara nne katika mwaka mmoja watatolewa katika orodha ya wenye shamba na lipeanwe kwa mtu mwingine.
  Wakulima wanaweza kuandikisha rufaa ya makumbusho ya shamba au kupokonywa shamba kwa kumwandikia Mratibu wa Mpango wa Mashamba. Rufaa hii itapitiwa na Mratibu wa Mpango wa Mashamba, Meneja wa Shamba wa mahali ambapo shamba linalozungumziwa lipo, na Meneja mwingine wa Shamba ambaye ni wa rangi/kabila moja na/au anayezungumza lugha sawa na mkulima (ikiwezekana).

Taarifa ya Kuondoa Hatiani:
Kwa kulipia au kupokea msaada wa kimasomo kwa ploti ya shamba la jamii, mhusika anakubali kufuata sera na taratibu za mpango na kulinda, kutetea na kuondoa hatiani Ofisi ya Bustani na Starehe (Parks and Recreation), Mpango wa Shamba la Jamii, Jiji la Portland, Mwenye Mali na wote waliokodisha, na maafisa, maajenti na waajiriwa wao kutokana na uharibifu, madai, mashtaka, vitendo vyovyote vinavyotokana na, au kwa sababu ya, uharibifu wowote wa mali au majeraha ya mwilini au kifo cha mtu yeyote kinachotakana na kuishi na/au mhusika, mkulima mwenza wa mhusika au wageni wake kutumia Shamba.

Taarifa ya ADA:
Ili kuhakikisha kwamba kuna usawa katika kupata mipango, huduma, na shughuli, Jiji la Portland litarekebisha sera na taratibu zake kwa makini na kupeana misaada michache na huduma kwa watu wenye ulemavu. Wasiliana na wafanyakazi wa Mpango wa Shamba la Jamii kwa 503-823-1612 (TTY 503-823-6868) ili kuomba maombi kama haya.

Taarifa ya Kutobagua:
Mipango na huduma za Portland Parks & Recreation huonyesha utofauti wa kitamaduni katika jamii yetu. Hatubagui watu kwa misingi ya dini, rangi, jinsia, nchi utokako, hisia za kimapenzi, umri au uwezo wa mtu.